

YESU NA MAMLAKA

“Kwa sababu ndio mlioitiwa; maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuata nyayo zake.” 1 Petro 2:21

Yesu aliacha kielelezo. Katika fungu la maandiko hapo juu, Yesu alituachia kielelezo cha namna ya kuhimili mateso. Pia, Yesu alionyesha jinsi ya kupenda, jinsi ya kujali, na jinsi ya kuwa wenye huruma. Alionyesha jinsi ya kuwa wakarimu, wema na wasamehevu. Bwana wangu ametuonyesha kila tunachokihitaji kukijua juu ya maisha. Majibu yapo, anatumo sisi tu, tusome Neno lake ili tupate majibu.

Mara kwa mara nashangaa kwanini watu wanayatazama maisha ya Yesu na kudai kuwa tunatakiwa kuzifuata nyayo zake katika mambo ya miiko na maadili. Lakini wakati huo huo linapokuja jambo la ukweli wa mafundisho, wengi huamini kuwa tuko huru kuamua na kufanya tunayotaka. Na hili ndilo lililopelekea kuandikwa kwa somo hili. Je, Yesu alikuwa huru kufanya lolote alilotaka, bila kujali mamlaka kuu (iliyo juu yake)? Je, alijua matashi ya Baba, na akajiamuria mwenyewe la kufanya? Je, Yesu aliuchukulia ukimya wa Baba kama ruhusa kutenda kwa kulingana na matashi yake?

Katika Injili ya Yohana, Yohana aliyezoeleka kama “Mtume wa Upendo,” aliandika kidogo juu ya Yesu na namna Yesu alivyoichukulia na kuikubali mamlaka.

Endapo leo tutakuwa kama Yesu, Kama tutazifuata nyayo zake katika mambo yote, basi tunapaswa kujua jinsi alivyoiheshimu mamlaka ya Baba.

Yesu alipokabiliwa na Mamlaka ya Baba, Je, alilia, alitupa, alibamiza mlango, aligoma kutii, alijifanyia mambo yake, alifikiri haijalishi, alifikiri nani atatilia maanani, Alifikiri ni yeye na anayotaka, na Je, alitafuta mwanya?

Yesu alikuwaje alipokabiliwa na mamlaka ya Baba? Kwa hakika kama kuna mwongozo unaopatikana katika maisha ya Yesu, basi mwongozo huo ni mamlaka kwetu leo. Hukubali? Hebu tujaribu, na tuone kama tunakubaliana na Yesu?

Yesu na Mamlaka ya Baba

1. Yesu alikuja kufanya mapenzi ya Baba na kutekeleza kazi ya Baba, Yohana 4:34. Je, na wewe waweza kusema hivyo hivyo?
 2. Yesu asingefanya lolote kwa matashi yake bila mamlaka ya Baba, Yohana 5:30. Je, kuna mamlaka ya Baba Katika yote unayoyafanya katika maisha yako na ibada?
 3. Katika huduma ya Yesu hapa duniani, Je, alitekeleza yote aliyoamuriwa kuyatenda? Yohana 5:36. Je, Unatekeleza yote ambayo Baba amekwambia uyafanye?
 4. Hivi, Yesu hakufundisha chochote bila “Asema Bwana” (Yohana 7:16). Je, na wewe unatafuta kwanza “Asema Bwana”. Ona Yesu anachosema juu ya wale wasitafuta kwanza “Asema Bwana.” “ Yeye anenaye kwa nafsi yake tu hutafuta utukufu wake mwenyewe;” Yohana 7:18.
 5. Yesu aliongea yale tu aliyosikia kwa Baba. Alifundisha yale tu ambayo Baba alimwagiza. Ndiposa daima alifanya yampendezayo Baba, maana alifanya tu aliyoagizwa na Baba Yohana 8:26-29. Vipi wewe? Katika mambo yahasuyo mamlaka ya biblia daima unaongea kama Baba alivyoongea? Je, daima unafundisha yale tu unayoyasoma na kuyathibitisha kwenye maandiko? Kama sivyo, utawezaje kumpendeza Mungu? Na kufanywa huru?
 6. Yesu hakufundisha kwa kadri ya maoni yake au hisia zake kamwe. Daima alisema aliloamuriwa, kwa kujua kuwa uzima wa milele umo katika maneno ya Baba (Yohana 12:48-50; Yohana 14:10). Vipi wewe? Je, unaruhusu maoni yako na hisia zako kuwa mwongozo wako? Je hisia zako na maoni yako ni “uzima wa milele”?
 7. Yesu alithibitisha upendo wa Baba kwa ulimwengu kwa kutenda yale yale amabayo Baba alimwamuru. Yohana 14:31. Vipi wewe? Unaamuriwa na Mungu kwa yote uyafanyayo katika maisha na ibada?.
- Kiini cha vifungu vyote hivi ni kwamba Yesu hakuacha maoni yake binafsi au hisia zake kuvuruga ambacho Baba alikuwa amemwambia afanye.

Alikuwa mtiifu hata mauti, Wafilipi 2:8. Pia, hakupitiliza kamwe mipaka aliyowekewa na Baba. Na Yesu hakusema wala hakuuchukulia ukimya wa Mungu kuwa ni ruhusa. Badala yake, Yesu alitufundisha, na kutuonyesha kwa kielelezo chake kwamba alifanya na angefanya aliyoelekezwa tu. Leo, linapokuja suala la mamlaka ya Biblia, fuata nyayo za Yesu, na yote yataenda vyema. Kaidi Mamlaka ya Yesu, kwa hakika utakuwa unafanya jambo ambalo Yesu mwenyewe alikataza. Wakolosai 3:17; Zekaria 10:12; Waefeso 5:10.